**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

*Simu: +255262963309/13/14*
*Nukushi: +255 262 963 316*
*Barua pepe: ps@lands.go.tz*
*Tovuti: www.lands.go.tz*

*Mji wa Serikali, Mtumba,*
*S. L. P. 2908,*
***40477* DODOMA.**

## TAARIFA KWA UMMA

Kumekuwepo na taarifa ambazo zimekuwa zikisambaa kwenye mitandao ya kijamii kuhusu kuvunjwa kwa nyumba iliyokuwa imejengwa kwenye Kiwanja Na. 318 Kitalu 'J' Mbezi, Manispaa ya Kinondoni. Taarifa zinaeleza aliyetekeleza zoezi la kuvunja anatajwa kuwa ni Bi. Jacqueline Noni.

Kumbukumbu zilizopo zinaonesha Kiwanja Na. 318 Kitalu 'J' Mbezi kilimilikishwa awali kwa Hati Milki iliyosajiliwa kwa Na. 29350 mwaka 1983 kwa muda wa miaka 33 kwa Ndugu Costa James Ninga wa S. L. P 2108 Dar es Salaam. Mwaka 1993 Ndugu Costa James Ninga alihamisha milki yake kwa njia ya mauziano kwenda kwa Bi Jacqueline Noni kwa gharama ya shilingi 500,000 na kibali cha uhamisho huo kupata kibali cha Kamishna wa Ardhi. Aidha, baada ya milki yake kuisha, ilihuishwa tena kwa miaka 99 kuanzia mwaka 2015.

Kiwanja hiki kimekuwa na mgogoro wa muda mrefu unaohusisha uvamizi uliofanywa na mlalamikaji na umekuwa ukishughulikiwa kiutawala katika ngazi mbalimbali za mamlaka ikiwemo ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni na Wizara. Aidha, wakati wa zoezi la kliniki ya ardhi katika eneo la Bunju lililoendeshwa na Wizara mwezi Februari na Machi 2024 wahusika kwenye mgogoro huu walipata fursa ya kusikilizwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi **Mheshimiwa Jerry William Silaa (Mb.)**.

Baada ya wahusika kusikilizwa na kupitia taarifa za umiliki, ilibainika kuwa mmiliki halali wa kiwanja tajwa ni Bi. Jacqueline Noni. Aidha, ilielekezwa ili kumaliza mgogoro huu, wahusika watekeleze yafuatayo:-

1) Mvamizi akubaliane na mmiliki kumlipa fedha;
2) Mvamizi amtafutie kiwanja kingine mmiliki; na
3) Mvamizi aondoshe jengo lake au avunjiwe kiwanja kiwe huru kwa mmiliki halali.

Maamuzi haya yalizingatia haki ya Bi. Jacqueline Noni ambaye kwa miaka 31 tangu alipomilikishwa ameshindwa kutumia mali yake halali kama Ibara ya 24 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Toleo la Mwaka 1977 inavyotaka badala ya kuangalia nyumba ya mvamizi iliyobomolewa.

Mwisho, umma wa watanzania unakumbushwa kuzingatia maelekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Ardhi wakati wa kuhitimisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Bungeni **kuwa kwa yeyote anayekalia kiwanja kisicho chake, akubaliane na mmilki halali kumaliza mgogoro uliopo**. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia haki za wamiliki wa ardhi kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Imetolewa na

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**
**1 JUNI, 2024.**